



# WEJISA COMPANY LIMITED

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

WEJISA COMPANY LIMITED

KITUO CHA KAZI/WORK STATION: DODOMA

Wejisa Company Limited, ni kampuni ya kizalendo iliyosajiliwa rasmi, inayobobe katika huduma za usimamizi wa taka na usafi wa mazingira. Misingi tunayoizingatia kama kampuni ndio nguzo kuu zilizojenga jina la Wejisa kama taasisi ya kuaminika na inayowajibika.

Kupitia kauli mbiu yetu: "Weka Jiji Safi" tumejjengea nafasi kama mshirika wa kweli kuhakikisha miji yetu inabaki salama muda wote. Kipaumbele chetu ni kutoa huduma bora za kuaminika na zinazojali mazingira, huku tukilenga kuwahudumia wateja wetu wote kwa kiwango cha hali ya juu. Kwa pamoja, tunajenga mazingira bora na salama kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

## 1. MSIMAMIZI MKUU (HEAD OF SUPERVISORS) – NAFASI 1

### Majukumu:

- Kusimamia wasimamizi wa kazi na kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao ipasavyo.
- Kurahisihsa mawasiliano kati ya menejimentibna wafanyakazi wa chini.
- Kuhakikisha kazi zote za usafi na bustani zinatolewa kwa ubora na kwa wakati.
- Kupanga na kugawa kazi kwa wasimamizi na timu nzima.
- Kufuatilia mahudhurio, nidhamu na utendaji wa wafanyakazi wote.
- Kutatua changamoto au malalamiko kutoka kwa wateja au timu ya kazi.
- Kutoa ripoti za kazi kila siku/wiki/mwezi kwa uongozi mkuu.
- Kuhakikisha vifaa vya kazi na usalama kazini vinatekelezwa kikamilifu.

### Sifa:

- Elimu: kuanzia kidato cha nne hadi stashahada
- Ujuzi mzuri wa uongozi na mawasiliano
- Uzoefu katika usimamizi kazi za usafi utapewa kipaumbele
- Umri: miaka 18 hadi 45

## **2. MSIMAMIZI WA USAFI (MSIMAMIZI WA WAFANYA USAFI)– NAFASI 2**

### **Majukumu:**

- Kugawa kazi kwa wafanyakazi wa usafi.
- Kusimamia utekelezaji wa usafi ndani na nje.
- Kukagua maeneo baada ya usafi.
- Kuripoti maendeleo ya kazi kwa msimamizi mkuu.
- Kuhakikisha matumizi sahihi ya vifaa vya usafi.
- Kuweka nidhamu na ushirikiano kazini.

### **Sifa:**

- Elimu kuanzia kidato cha nne (Form IV)
- Uzoefu wa kazi ya usimamizi ni faida
- Umri: miaka 18 hadi 45

## **3. MFANYAKAZI WA USAFI NDANI NA NJE (CLEANERS) – NAFASI 20**

### **Majukumu:**

- Kufanya usafi wa ofisi, madirisha, sakafu na vyoo.
- Kusafisha maeneo ya nje kama parking, korido.
- Kutunza na kutumia vifaa vya usafi kwa usahihi.
- Kuondoa taka na kuzitupa katika maeneo maalum.
- Kuhakikisha mazingira yanabaki safi muda wote.
- Kufuata maelekezo ya supervisor kila siku.

### **Sifa:**

- Elimu kuanzia darasa la saba na kuendelea
- Uzoefu wa kazi ya usimamizi ni faida
- Umri: miaka 18 hadi 45

## **4. MTUNZA BUSTANI (GARDENER) – NAFASI 10**

### **Majukumu:**

- Kupanda, kumwagilia na kutunza mimea, maua na nyasi.
- Kupogoa miti na kuchoma au kuondoa majani yaliyooza.
- Kupalilia na kuweka mbolea kwenye bustani.
- Kudumisha usafi wa mazingira ya bustani na barabara za nje.
- Kutumia na kutunza vifaa vya bustani kwa usalama.
- Kuripoti matatizo yoyote ya bustani kwa msimamizi.

### **Sifa:**

- Elimu kuanzia darasa la saba na kuendelea
- ‘Weka Jiji Safi’  
Specialized in Waste Management

- Uzoefu wa kazi ya usimamizi ni faida
- Umri: miaka 18 hadi 45

#### JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

##### Viambatanisho:

- Barua ya maombi
- Wasifu binafsi (CV)
- Namba ya simu ya mawasiliano

Tuma Maombi Kupitia barua pepe: [brigitamacha@wejisa.co.tz](mailto:brigitamacha@wejisa.co.tz) / [info@wejisa.co.tz](mailto:info@wejisa.co.tz)

Mwisho wa kutuma maombi: 8/09/2025

##### Maelezo ya ziada:

- Wanawake wanahamasishwa kuomba
- Ni waombaji walikidhi vigezo pekee watakaowasiliana kwa hatua Zaidi
- Kazi zitatolewa kwa walio tayari kuanza mara moja.